CRDB BANK

*Tunakusikiliza*

# TAARIFA YA MABADILIKO YA MAHALI UTAKAPOFANYIKA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA NANE WA WANAHISA WA BENKI YA CRDB

Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba wa Wanahisa wa Benki ya CRDB uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 21 Mei 2022 uliazimia kuwa, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nane wa Wanahisa wa Benki ya CRDB ufanyike siku ya Jumamosi **tarehe 20 Mei, 2023 Makao Makuu ya Benki ya CRDB, Dar es Salaam.**

Ili kuendana na mkakati mpya wa Benki wa 2023 – 2027, Bodi ya Wakurugenzi ilijadili upya na kuridhia kuhamisha Mkutano Mkuu wa ishirini na nane kutoka Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam kwenda katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) kwenye Ukumbi wa Simba.

Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza mabadiliko hayo kwa wanahisa wanaomiliki zaidi ya asilimia hamsini ya hisa za Benki kwa mujibu wa Katiba ya Benki na Sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002, na Wanahisa hao wameidhinisha mabadiliko hayo.

Hivyo basi, Wanahisa wote wa Benki ya CRDB wanataarifiwa kwamba Mkutano Mkuu wa ishirini na nane wa Wanahisa wa Benki ya CRDB utafanyika katika Ukumbi wa Simba uliopo Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) siku ya Jumamosi tarehe 20 Mei, 2023.

**KWA IDHINI YA BODI**

J.B. Rugambo
KATIBU
14/4/2023